Idara ya Watoto na Familia
Kitengo cha Huduma kwa Familia
280 State Drive
HC 1 North Bldg B
Waterbury, VT 05671-1030

Wakala wa Huduma kwa Wanadamu

Machi 19, 2020

Mpendwa Mlezi wa Jimbo wa Vermont,

Kwa vile wewe ni familia inayotoa utunzaji na usaidizi unaohitajika kwa watoto wetu wanaohitaji usaidizi na familia zao, unategemewa kila siku. Tunakuthamini na kukushukuru kabisa kwa rehema zako na utunzaji wako ambao umeonyesha katika hali iliyoko sasa na inayoendelea katika jamii yetu tunapopambana na mlipuko wa ugonjwa wa kuambukizwa wa *COVID-19*. Tunajua kwamba kufungwa kwa shule na sehemu za utunzaji wa watoto huleta changamoto zaidi kwa walezi. Tunashirikiana na Ofisi za Wilaya yetu ili kutambua na kushughulikia mahitaji yako.

Tunaelewa kwamba hali hii inamfanya mtu awe na maswali mengi sana. Kitengo cha Huduma kwa Familia kitatumia tovuti ifuatayo ili kuwasilisha habari kwako, washirika wetu, na familia ambazo tunahudumia.

https://dcf.vermont.gov/fsd/COVID19

Idara ya Afya ya Vermont imeunda tovuti madhubuti ambayo huwa inasasishwa saa 2 mchana kila siku. Hapa ndipo pahali pazuri zaidi pa kupata habari mpya kuhusu maswali mahususi ya COVID -19. Tunajaribu sana 'tusikate na kubandika' habari kutoka kwenye tovuti hii kwa vile habari inabadilika badilika kwa kila siku.

https://www.healthvermont.gov/covid

Utapata majibu ya maswali mengi hapa, kama vile:

1. *Je, ni tahadhari gani ambazo ninaweza kuchukua ili nijilinde kutokana na COVID-19?*
2. *Je, dalili za COVID-19 ni gani?*
3. *Je, nitafanyaje ikiwa mtu kazini mwangu au katika familia yangu atakuwa mgonjwa?*
4. *Je, nitafanyaje ikiwa mtu kazini mwangu au katika familia yangu atapatikana kuwa na COVID-19?*

Mpigie simu daktari wako wa huduma ya msingi ikiwa mtu yeyote katika nyumba yako amekuwa mgonjwa. Ripoti ugonjwa wowote ulio na dalili za COVID-19 kwa Idara ya Afya ya VT kwa (802) 863-7240. Pia, mjulishe Mfanyakazi wa Huduma kwa Familia ikiwa mtu yeyote katika familia yako amekuwa mgonjwa.

5. *Je, ninaweza kupata habari au kuwasiliana kwa njia gani?*

Tunakuhimiza uwasiliane au upate habari kadri uwezavyo kufuatia mapendekezo yaliyopo sasa ya kukaa

mbali na watu. Baadhi ya Mashirika ya Wazazi Walezi yana kurasa za Facebook zinazotumika ambapo habari kuhusu vifaa na usaidizi zinapatikana. Tumepata kujua kwamba baadhi ya walezi wanaungana pamoja na "familia ya ushirika" ambazo kwa kawaida huwa ni ushirika mmoja wa kijamii. Kwa kushirikiana, mkiwa wachache, familia wanatimiza mahitaji ya kila mmoja — kwenda dukani kununua mboga, dawa n.k.

6. *Nina wasiwasi kuhusu matatizo ya kifedha kwa familia yangu?*

Tunaelewa kwamba janga hili huenda likaleta tatizo la kifedha kwa familia yako. Tunashirikiana na Ofisi yetu ya Biashara ili kukutafutia misaada ya ziada ya kifedha katika hali hii ya dharura. Mengi yatakuja baada ya muda mfupi.

Idara ya Kazi ya Vermonti imeelekezwa na amri ya Gavana ipatiane bima ya kutoajiriwa kwa Wanavermont ambao wanafuata maagizo ya wahudumu wao wa afya ya kujitenga au kujikarantini.

7. *Je, nikiwa na jambo la dharura baada ya saa za kufanya kazi?*

Mpango wa Huduma ya Dharura (ESP) wa Kitengo cha Huduma kwa Familia utaendelea kufanya kazi masaa 24/7. Unaweza kuwasiliana na ESP kwa 1(800)649-5285. Tutakuwa tunahimiza watoto wapunguze matembezi ya hapa na pale katika wakati huu kwa mujibu wa kufuata miongozo ya Idara ya Afya ya Vermont.

Tunaelewa kwamba huenda ukawa na wasiwasi kuhusu kumleta mtoto mgeni katika nyumba yako wakati huu. Tunafanya kile tunachokiweza ili kuwaweka watoto pahali wanapopajua, wakitunzwa na walezi wanaowajua. Kuna nyakati zingine ambapo hii haitawezekana. Wafanyakazi wetu wameelekezwa wamuulize kila mteja ambaye tunakutana naye baadhi ya maswali ya kukagulia kwa *COVID-19*. Isitoshe, mtoto atatumwa kwa daktari wake wa huduma ya msingi ili achunguze afya yake na kuamua ikiwa anapaswa kupimwa *COVID 19* wakati ambapo jibu la swali la uchunguzi ni "ndiyo".

8. *Je, bima ya Medicaid inagharamia gharama za COVID-19?*

Watoto ambao wako chini ya malezi wanalipiwa gharama na Medicaid. Upimaji wa *COVID-19* unalipiwa. Isitoshe, baadhi ya dawa za kunuliwa dukani pia huenda zikalipiwa na Medicaid.

9. *Je, miongozo kuhusu kukutana kwa mzazi na mtoto ni gani?*

Kukutana kwa mtoto na mzazi kulisimamishwa kwa muda wa masaa 48 kuanzia 03/17/2020 hadi 03/18/2020 ili kupanga jinsi ya kuendelea na shughuli katika hali hizi za sasa. Kuanzia 03/19/2020 mwongozo ufuatao ndio wa kufuatwa:

Wakati ambapo mtoto ameondolewa kwa mzazi na kuwekwa kwa malezi ya Idara ya Watoto na Familia (DCF), kukutana kwa mtoto huyo na mzazi huwa kunaamuriwa na mahakama, na Idara ya Watoto na Familia (DCF), kama mlezi, ina jukumu la kuhakikisha kwamba wamekutana. Wakati huo huo, wakati huu wa janga la *COVID-19*, Idara ya Watoto na Familia (DCF) ina jukumu la kuhakikisha kwamba mzazi na mtoto wanakutana kwa njia salama na inayofaa, kulingana na mwongozo mpya kabisa kutoka kwa Idara ya Afya, na kwa kufuata matarajio ya mahakama.

Kuanzia sasa hivi, tutashughulikia na kusaidia kikamilifu kwenye simu kati ya wazazi na wazazi walezi (au walezi ambao ni wafanyakazi) wa watoto/vijana walio chini ya malezi ya Idara ya Watoto na Familia (DCF) ili kuhakikisha kwamba kukutana kati ya mzazi na mtoto kunafanyika kwa njia salama na inayofaa. Hii

itamaanisha kwamba watawasiliana wakiwa mbali katika hali nyingi.

Mipango ya kina ya kila mara ya kuwasiliana na watoto wakiwa mbali itaundwa na kuandikwa, na wapatanishi watawasiliana na wazazi kupitia mawasiliano ya mitandao kuhusu mpango ulioandikwa wa kuwasiliana na watoto wakiwa mbali. Mawasiliano haya ya mitandao yatajumuisha maagizo kwa wazazi kwamba wanapaswa kuzungumza na wakili wao kuhusu mambo haya, na mpango wa mwisho ambao watu wamekubaliana utaandikwa na kusambazwa kwa wahusika wote.

Mipango hii itaundwa na kuandikwa ili itumike katika kipindi hiki ambacho Vermont iko katika hali ya dharura. Kwa sasa kipindi chenyewe ni cha kuanzia 3/19/20 hadi 4/15/20.

Wazazi wataambiwa baadhi ya njia ambazo mawasiliano kati yao na watoto yanaweza kutendeka (k.m. moja kwa moja, kupitia simu, Skype, n.k...), ikiwemo wanapaswa kuwasiliana na watoto kwa muda gani na mara ngapi ambayo itakuwepo kwenye mpango. Njia ya mawasiliano inayopendelewa na kuhimizwa itakuwa njia ya kutokutana. Kabla ya mtoto na mzazi kukutana ana kwa ana vitu vifuatavyo vitazingatiwa:

- hakuna yeyote kati ya watu hawa wanaohusika katika kukutana huku (mzazi, mtoto au mlezi) ambaye amekaribiana na mtu ambaye ako na *COVID-19*,
- hakuna mtu yeyote kati ya wanaokutana ambaye amekuwa mgonjwa na akaonyesha dalili za mfumo wa kupumua katika siku chache zilizopita,
- hakuna yeyote kati ya watu hawa wanaohusika katika kukutana huku (mzazi, mtoto au mlezi) au mtu yeyote ambaye ako katika nyumba zao ambaye anahisi kwamba ako katika kundi la watu ambao wanaaminiwa kwamba wako katika hatari kubwa ya kuathirika endapo wataambukizwa *COVID-19*

Katika hali ambazo mzazi bado anaendelea kuomba kukutana ana kwa ana na kuna ushahidi wa kukutana na mtu aliye na *COVID* au aliye kwa hatari, FSD itaiomba mahakama iamuru mawasiliano ya simu au ya mitandao.

Tunaelewa kwamba vigezo vilivyotajwa hapa juu huenda visishughulikie matatizo yako yote kuhusiana na kukutana kwa mzazi na mtoto katika nyumbani kwako na familia yako. Tafadhali shirikiana na ofisi ya wilaya iliyoko karibu ili kushughulikia hali yako mahususi.

10. *Je, na kuhusu kukutana kwa ana kwa ana na Mfanyakazi wangu wa Huduma kwa Familia kila mwezi (FSW)?*

Ziara za kila mwezi za Ana kwa Ana kati ya watoto au vijana chini ya malezi wanaoishi katika makazi ya walezi au ya jamaa zimesimamishwa kwa muda katika kipindi hiki cha hali ya dharura katika Jimbo la Vermont (kwa sasa hadi Aprili 15, 2020) isipokuwa ikiwa kuna shaka kuhusu usalama wa mtoto au kijana huyo. Wafanyakazi wa Huduma kwa Familia bado wanahitajika kuwasiliana na kila mtoto angalau kila mwezi.

11. *Je, nitashughulikiaje miadi zilizopangiwa mtoto ninayemlea?*

Kwa miadi za tiba, baadhi ya madaktari wanaanza kuwahudumia wagonjwa kwa njia ya kutokutana. Wasiliana na mhudumu wako wa afya ili ujue ikiwa hii itawezekana. Ndicho hiki kiungo cha Wakala Mahususi za Afya ya Akili: https://mentalhcalth.vernont.gov/services/emergency-services/how-get-help

Kwa miadi ya kawaida ambayo si ya haraka, tunapendekeza kwamba zipangwe upya ili kupunguza uwezekano wa maambukizo. Tumesikia kwamba sehemu za matibabu ya watoto katika kliniki zimefungwa. Tafadhali hakikisha kwamba umewasiliana na daktari wako wa huduma ya msingi kabla ya kuenda kwenye kituo cha huduma ya haraka, tena kufanya hivi ni kuzuia kungoja sana pahali ambapo kuna uwezekano wa kuwa na wagonjwa.

12. *Je, kuna rasilimali nzuri ambazo zitanisaidia kujibu maswali ambayo watoto ninaowalea wanaweza kuuliza kuhusu Virusi vya Corona?*

https://www.nctsn.org/sites/default/files/resources/factsheet/outbreak_factsheet_1.pdf?fbclid=IwAR02_xh6JTvFs34K2q_w38m2AbywAx4JTajSw7NEAdsoX43YdmWeoLzQvgg

Tunafahamu kwamba baadhi ya walezi hawana barua pepe, hawajapatiana anwani yao ya barua pepe kwa Kitengo au wamebadilisha anwani zao za barua pepe na bado hawajapatiana habari zao mpya za mawasiliano kwa Kitengo. Ikiwa unamjua mtu ambaye huenda ako katika hali hii, tafadhali wasilisha habari hizi.kwake. Pia, kwa watu ambao wanahitaji kubadilisha anwani ya barua pepe au kupatiana anwani mpya ya barua pepe kwa Kitengo, tafadhali tumeni Majina yenu ya Kwanza na ya Mwisho na barua pepe zenu kwa Mkurugenzi wa Kitengo wa Mfumo wa Huduma, Barb Joyal kwa: Barbara.Joyal@vermont.gov

Mwisho, ningependa kuwashukuru nyote kwa kujitolea kwenu kutimiza mahitaji ya Wanavermont wetu ambao wanahitaji msaada kabisa. Tuko pamoja kwa hii hali!

Mwaminifu,

[SAHIHI]
Christine Johnson
Naibu Kamishna
Kitengo cha Huduma kwa Familia Idara ya Watoto na Familia (DCF)